



© KCCB-CPIHD - Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani, 2025

Ubunifu na utayarishaji:

Makao Makuu ya Baraza la Maaskofu Wakatoliki wa Kenya

Idara ya Kikatoliki ya Haki na Amani

Wahariri: Eusebius Atamallo, Festus Rotich and Wainainah Kiganya

Uchoraji: Robert Kambo

Usanifu na upambaji wa kurasa: Kelvin Malombe

Mratibu wa michango: Constance Ikhabu Mutende

Wapigaji chapa: Kolbe Printing Press,S.L.P. 468 Limuru 00217, Kenya

KENYA TUNAYOITAMANI

KAMPENI YA KWARESIMA 2025

YALIYOMO

- 5 **DIBAJI: KENYA TUNAYOITAMANI**
8 **UTANGULIZI: KWARESIMA KATIKA KANISA KATOLIKI**
9 **UFAFANUZI: VITUO VYA NJIA YA MSALABA**
13 **WIKI YA KWANZA - FAMILIA: MSINGI WA KANISA LETU NA JAMII**
13 TAZAMA: SIMULIZI
13 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
14 TAFAKARI YA KIROHO
15 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
15 KUJICHUNGUZA
15 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
17 **WIKI YA PILI - UFISADI**
17 TAZAMA: SIMULIZI
17 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
19 TAFAKARI YA KIROHO
20 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
20 KUJICHUNGUZA
20 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
22 **WIKI YA TATU - VIJANA: RASILIMALI ISIYOTUMIKA IFAAVYO**
22 TAZAMA: SIMULIZI
23 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
24 TAFAKARI YA KIROHO
25 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
25 KUJICHUNGUZA
25 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
27 **WIKI YA NNE - WAJIBU WA ELIMU YA MKABALA WA JUMLA**
27 TAZAMA: SIMULIZI
27 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
29 TAFAKARI YA KIROHO
30 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
30 KUJICHUNGUZA
30 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
32 **WIKI YA TANO - UTUNZAJI WA MAKAO YETU SOTE**
32 TAZAMA: SIMULIZI
32 AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI
33 TAFAKARI YA KIROHO
34 TENDA: MASWALI YA KUWAZIA
34 KUJICHUNGUZA
34 MATENDO YALIYOPENDEKEZWA
35 **MICHANGO YA 2024 YA KAMPENI YA KWARESIMA**
64 **SALA YA KUMTAKIA MTUMISHI KADINALI OTUNGA**
KUTANGAZWA KUWA MTAKATIFU
65 **SALA YA KAMPENI YA KUPAMBANA NA UFISADI**
66 **MUHTASARI**

KENYA TUNAYOITAMANI

Matamano huleta msukumo mkubwa ambao hushawishi matendo yetu mengi, mawazo na, hatimaye maisha yetu. Kidunia na kidini, matamano yana jukumu muhimu katika maamuzi yetu maishani.

Mara nyingi, matamano ya jamii za ulimwengu hujitokeza wazi kwa kutaka sana ufanisi wa mali na pesa, starehe na raha za kibinafsi ama kutosheleza haja za kila mtu binafsi. Matamano husukuma watu kutimiza malengo, kupata wanayoyahitaji na kuridhika. Lakini kidini, matamano yana maana ya ndani na ya kiroho. Kwa Wakristo, kutamani sio tu kutosheleza mahitaji binafsi lakini ni hamu kuu ya kutimiza mapenzi ya Mungu duniani kama yanavyotimizwa mbinguni. Ni kutamani utakatifu, unyoofu na kuishi kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu. Tunakumbushwa katika Mika 6:8 kwamba: “Yeye amekuonyesha yaliyo mema; na Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, na kupenda rehema, na kwenda kwa unyenyekevu na Mungu wako!” Kutamani yanayolingana na haki, huruma na unyenyekevu hutuelekeza kutimiza mapenzi ya Mungu. Lakini yasipolingana, matamano yanaweza kumsukuma mtu kwa ubinafsi na dhambi. Matamano ya Kikristo huonekana wazi kwa yanavyosukumwa na mapenzi kwa Mungu na majirani, yakilenga kutenda mema kwa manufaa ya wote.

Katika Biblia, matamano ni jambo la kutatanisha. Maandiko yanazungumzia jinsi tamaa hutujia kwa njia nyingi; yanaweza kuwa hisia ya kimaumbile, chanzo cha majaribio ama nguvu inayoweza kumwelekeza mtu kwa utakatifu au dhambi. Katika Mwanzo 3:6, matamano yanajitokeza kwa mara ya kwanza wakati Hawa alipoona ya kuwa ule mti ulifaa kwa chakula, ulipendeza macho na kutamanika kwa maarifa. Tamaa hiyo ndiyo ilimletea mwanadamu laana ya Mungu. Kwa upande mwingine, Biblia inawasilisha matamano kama jambo takatifu na adilifu. Katika Zaburi 37:4, wanamtumaini Bwana, wanatenda mema na kupendezwa na uaminifu, wanaahidiwa kuwa wajifurahishe katika Bwana, naye atawatimizia haja za moyo.

Tunapojiandaa kwa Kampeni ya Kwaresima ya 2025, maudhui **Kenya Tunayoitamani** yana mguso maalumu kwa Wakristo wote nchini. Tunaitamani Kenya isiyo na migawanyiko, ufisadi au kuvunja watu mioyo lakini nchi ambapo haki, amani na umoja zinatawala; rai wote, hasa waliotengwa ama kubaguliwa, wanaweza kupata mafanikio,

mahala ambapo uongozi una sifa ya uadilifu na kila mmoja anajali maslahi ya mwingine.

Tunaalikwa katika msimu huu wa Kwaresima kutafakari kwa kina kuhusu tunayotamani kwa nchi yetu na kujiuliza iwapo matamania hayo yanalingana na maadili ya ufalme wa Mungu. Tunapaswa kutamani mabadiliko yanayoanzia nyoyoni zetu na kusambaa katika mfumo wa jamii. Msimu huu wa Kwaresima tunaalikwa kuchunguza tunayoyotamani na kuyatakasa. Kenya inakabiliwa na changamoto nyingi – misukosuko ya kisiasa, matatizo ya kiuchumi, na uvunjaji wa haki za jamii – na tunaombwa kutamani yaliyo mema kwa nchi, tuombe uponyaji na umoja, na tujitolee kutekeleza mambo yanayoangazia matamania hayo. Wakristo hawafai kuiombea tu Kenya lakini kutafuta kuimarisha haki katika kila nyanja ya taifa. Raia ni lazima wawe tayari kushirikiana kujenga taifa lenye haki na amani ambazo Kristo anatakia watu wake.

Tunapohitajika kuchukua maamuzi magumu ilhali hatua sahihi inayohitajika si bayana, tunapaswa kuongozwa na mafundisho ya Mtakatifu Thomas Aquinas, *Doctrine of Double Effect*. Mafundisho hayo hutuhimiza kuwa kila tunapokabiliwa na hali yo yote ambapo matokeo ya matendo yetu yanaweza kuwa na manufaa na madhara kwa pamoja, hatuna budi kuchunguza kikamilifu malengo yetu. Iwapo tunatamani mema kwa dhati lakini yatokee mabaya bila sisi kukusudia, matendo yetu yanaweza kukubalika kuwa ya dhati. Kwa mfano, katika kulinda haki, huenda tukajipata katika hali ambapo utekelezaji sheria unamwumiza mwingine. Katika hali kama hiyo, tunapaswa kuongozwa na nia yetu ya kuhakikisha manufaa kwa wote. Mtakatifu Thomas anatukumbusha kwamba ni lazima matendo yetu yalingane na majukumu yanayojali uadilifu ili kutenda haki, kwa busara na kwa mapenzi ya Mungu.

Msimu wa majuma matano wa Kwaresima unawasilisha mada tano za **Kenya Tunayoitamani** ambazo zitatusaidia kujenga matamania yetu kwa nchi. **Wiki ya kwanza** tunaangazia **umoja wa familia na jukumu lake katika kujenga jamii yenye amani**. Familia ni shule ya kwanza ya kufundishia maadili; familia iliyoungana hujenga taifa lenye umoja. Tunashughulikia suala la **ufisadi na haja ya uwajibikaji** katika **wiki ya pili**. Matarajio ya kuwa na Kenya isiyo na ufisadi yanapaswa kueneza mizizi ndani mwa kila mmoja wetu. Tunaalikwa katika **wiki ya tatu** kutafakari kuhusu **vijana na uwezo walio nao** na ambao haujatumika kikamilifu nchini. **Wiki ya nne** tunachunguza umuhimu wa **elimu inayojali nyanja zote za maisha**, tukitamani kuwa na mfumo unaotilia mkazo mafundisho yanayonoa fikira na kujenga tabia. Tunamalizia **wiki ya tano** kwa kuangazia **umuhimu wa kutunza makao yetu**

sote. Tunahimizwa kutafakari kuhusu tunavyotamani usimamizi wa mazingira uwezao kurejesha na kulinda vyote vilivyoubwa na Mungu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Ujumbe wa kila wiki unampatia kila mmoja na jamii yote changamoto. Tunapotafakari kuhusu **Kenya Tunayoitamani**, tunahimizwa kufikiri siyo tu tunayoyahitaji sisi lakini pia tunayowatakia wengine. Tunaombwa kutamani mema ya kila mtu, bila kujali asili au tabaka zao. Tukiwa Wakristo hatuwezi kuridhika na baraka za binafsi ilhali wengine wanateseka. Tuna jukumu la kuhakikisha manufaa kwa wote na hatuna budi kutamani jamii inayoendeleza usawa, haki na upendo. Changamoto tuliyonayo siyo tu kutamani mabadiliko ya kiroho lakini kujitolea kwa dhati kutenda. Jukumu letu tukiwa raia wa Kenya ni kujenga nchi tunayoitamani. Kazini, katika siasa, kwenye jamii na hata nyumbani, hatuna budi kudumisha uadilifu, upendo na haki. Injili inatutaka tuwe chumvi na nuru ya ulimwengu; tuwe maajenti wa kuiboresha Kenya.

Safarini ya msimu huu wa Kwaresima, tutafakari maneno ya mwizi 'mwema' ambaye pia alisulubiwa msalabani aliyesihi: "Ee Yesu, nikumbuke utakapoingia katika ufalme wako (Luka 23:42). Hata nasi tutakase matamano yetu na kuhakikisha yanalingana na ya ufalme wa Mungu, tukiangazia mema ya wote, hasa waliotengwa, waliokandamizwa na wasio na sauti.

Hatimaye, tumgeukia Mama Maria aliye mfano kamili wa kutamani mapenzi ya Mungu. Sala anazotutolea, sisi wanawe, ziongoze matamano yetu na kutuletea Kenya yenye ,mafanikio, haki na huruma. Kwa sala zetu, kupitia kwa Mama Maria, zituwezeshe kufahamu matamano kamili ya Mungu kwa taifa letu na tushirikiane kuhakikisha yanatimia. Amina.

Muwe na Kwaresima iliyobarikiwa.



Askofu Simon Peter Kamomoe

Mwenyekiti, KCCB-CPIHD

Idara ya Kikatoloki ya Haki na Amani

KWARESIMA KATIKA KANISA KATOLIKI

Kwaresima ni kipindi cha siku 40 cha kufunga na kujinyima, kusali na kutubu kabla ya Pasaka. Kulingana na utamaduni wa Kikristo, msimu huu katika mwaka wa kiliturjia huanza Jumatano ya Majivu na kumalizika Jumapili ya Matawi. Ni adhimisho la kila mwaka ambalo huwatayarisha waumini – kupitia sala, toba, kutoa zaka na kujinyima – kwa matukio yanayohusiana na mateso ya Yesu msalabani, na maadhimisho ya ufufuko wake. Wakatukumeni hubatizwa Jumapili ya Pasaka.

Kwa nini siku 40?

Nambari 40 ni muhimu katika maisha ya Wakristo. Musa na wana wa Israeli, kwa mfano, walitanga jangwani kwa miaka 40 wakijiandaa kwenda katika nchi waliyoahidiwa na Mungu. Musa alikaa juu ya Mlima Sinai kwa siku 40 bila kula wala kunywa alipokuwa ameenda kupokea vibao vya mkataba ambao Mungu aliwawekea Waisraeli. Nyakati za Nuhu, gharika iliendelea kwa siku 40 mchana na usiku. Eliya alikaa siku 40 mchana na usiku juu ya Mlima Horebu bila chakula. Yesu naye alienda jangwani na kufunga kula na kunywa kwa siku 40 mchana na usiku.

Asili ya Kampeni ya Kwaresima Kenya

Kuzingatia wito wa kiroho wa msimu wa Kwaresima, Kanisa Katoliki katika Kenya liliazimia kuwapasha waumini habari kuhusu matatizo yanayokumba jamii na kushirikiana nao kutetea mabadiliko. Kupitia kwa Kampeni ya Kwaresima, Maaskofu wa Kanisa Katoliki huwaita Wakristo wote na watu wa mapenzi mema kuungana na kukabiliana na matatizo hayo, huku wakitetea mabadiliko. Kwa kuungana na maaskofu katika utetezi huo wa mageuzi, juhudi za kila mtu binafsi pamoja na sauti ndogo ya kila mmoja ikiunganishwa na ya wengine husikika mbali, nayo matendo ya kila mmoja huongezeka yakijumuishwa na ya wengine.

VITUO VYA NJIA YA MSALABA

KITUO CHA 1: Yesu ahukumiwa kifo

Tunamwona Yesu akiwa amevishwa taji la miiba kichwani akitokwa na damu, huku mikono yake imefungwa kutoka nyuma. Nguo zake zimeshikana na vidonda vyake. Pilato anachukua maji na kunawa mikono yake mbele ya umati wa watu akisema: "Sina hatia juu ya damu ya mtu huyu, hili ni jukumu lenu!" Sisi pia hufanya vivyo hivyo. Tunawafunga wengine kwa maoni yetu na kuwadhalilisha kwa kutumia vibaya mamlaka yafaayo kuwainua wala si kuwaingiza utumwani. Tunaomba kuwa walio mamlakani wasitufunge mikono na kutuzuia kuinua maisha yetu.

KITUO CHA 2: Yesu aubeba msalaba wake

Tunatafakari kuhusu uzito wa msalaba na jinsi unavyoauumiza mabega yake baada ya kupewa hukumu ambayo haikustahili. Ni mara ngapi huwa tunawabebesha mizigo mizito marafiki zetu na wengine walio karibu nasi kwa matendo yanayosababisha usumbufu kama vile uchafuzi, utumiaji mbaya wa mali asili, kutupa ovyo takataka na kuharibu vianzo vya maji safi na salama ya kunywa? Tuombe tuwe wasimamizi bora wa mali tulizopewa na Mungu kutunza kwa manufaa ya wote.

KITUO CHA 3: Yesu anaanguka kwa mara ya kwanza

Tunaushuhudia unyonge unaojionyesha katika macho yake, mwili wake uliochoka hadi akaanguka chini, huku akihangaishwa na askari wakijaribu kumwinua. Sisi pia hujipata katika hali sawa maishani. Kuna masuala yanayotubwaga chini kama vile changamoto za gharama ya juu ya maisha zinazotuzidishia magunu maishani. Yesu anatupatia nguvu za kuichunguza hali yetu kwa matumaini. Tuombe kuwa walio na uwezo wawasaidie maskini na walio mamlakani washughulikie gharama ya juu ya maisha inayowalemea maskini.

KITUO CHA 4: Yesu akutana na mamake

Tukiwatazama, tunatafakari kuhusu muujiza wa uwezo wa upendo kumpatia mtu nguvu za kushinda masaibu ya maisha, vurugu, chuki, utengano na kukata tamaa. Ni mara ngapi huwa tunawaonyesha upendo watu wakiwa katika hali mbaya, wanapokataliwa, kueleweka vibaya, na hata kusingiziwa maovu bila hatia au kutoka kwa familia ambazo baadhi ya watu wake wana imani kali za dini zinazowaathiri wengine? Tuombe tusaidiwe kuepuka ubaguzi kwa misingi ya dini; kwamba kwa vile sote tumeumbwa kwa mfano wa Mungu, tunapaswa kujiepusha na maovu kama vile ulanguzi wa binadamu, kung'oa watu viungo vya mwili na imani kali za dini. Tuombe tupate uwezo wa kuwaona wengine wote kuwa viumbe wa Mungu, tupendane, tutambue na kulinda utukufu wa maisha.

KITUO CHA 5: Simoni wa Kirene amsaidia Yesu kuubeba msalaba

Tunautazama uso wake uliojaa huzuni kana kwamba anaomba msaada wetu, huku tukitafakari kuhusu mateso anayopitia. Ni muhimu kutambua jinsi anavyomtazama Simon kwa unyenyekevu na shukrani. Yesu anatumkumbusha kuwa kuna nyakati tunahitaji misaada ya wengine bila kushuku nia zao. Tunahimizwa kuingia katika maisha ya wanaopitia magumu wakijaribu kukimu maisha, wale ambao familia zao zimo katika hatari ya kusambaratika na walionyimwa hadhi ya binadamu. Tunaalikwa kudumisha mshikamano na kutambua nguvu za umoja kwa manufaa ya familia zote, wenye tatizo la utumiaji mbaya wa dawa za kulevyu, au wanaoshiriki umalaya na maovu mengine yanayokumba familia.

KITUO CHA 6: Veronica ampangusa Yesu usoni

Tunaona nini tunapoutazama uso wa Yesu? Unatuonyesha nini? Tunaona nini tunapotazama kwa undani dhiki na machungu ya wengine? Tunaweza kuwakubali walio taabani? Waliofunikwa uso kwa dhiki na machungu?

KITUO CHA 7: Yesu anaanguka kwa mara ya pili

Tunamtazama Yesu akiwa chini na kutafakari machungu anayoyapitia. Tunamwonea huruma na kufahamu kwamba hatutawahi kamwe kujiona tukiwa pekee yetu tukikabiliwa na mateso. Tumwombe atusamehe kwa kukosa kumtegemea. Ee Mungu, tupe nguvu za kutuwezesha kukabiliana na wasiwasi, huzuni, machovu, matatizo ya akili na magonjwa. Tuendeleo kukutegemea kama asili ya matumaini ili tuzidi kukutumikia ipasavyo.

KITUO CHA 8: Yesu akutana na wanawake wa Yerusalemu

Tunapotazama nyuso zao, tunaona zilivyojaa upendo na shukrani, majonzi na woga. Tunashangazwa na yaliyofanyika kati yao. Upendo wake uliojaa huruma kwetu unatuweka walipo wanawake na watoto waliomwonyesha upendo na huruma. Bwana, wanawake wa Yerusalemu wanatumkumbusha kwamba hata wanaoteseka wana hadhi na ni wanao. Tunaomba utuwezeshe kurejesha thamani ya utu bila kuhusudu mali, teknolojia, serikali, rangi ya ngozi, asili na matendo mengine yanayoharibu sura ya ulimwengu.

KITUO CHA 9: Yesu aanguka kwa mara ya tatu

Tunatafakari kuhusu hali yake akiwa chini; mateso yanayotufanya sisi kukamilika, jinsi alivyokubali hali yake ili kutupatia uhai. Tunatafakari ili kupatana na kuupokea upendo wake kamili. Amejitolea kabisa kwetu. Bwana, tuwezeshe kufuata maagizo yako ya huruma, ukarimu na upendo. Mara nyingi huwa tunapuuzwa maagizo hayo. Tunakuomba utuonyeshe njia yako ili ibaki kuwa chanzo cha nguvu zetu katika matatizo na mateso.

KITUO CHA 10: Yesu anapokonywa mavazi yake

Tunashuhudia akivuliwa mavazi na kukabiliana na mauti akiwa uchi. Tunatafakari anavyojifichua kwetu, bila kuficha chochote. Bwana, umetualika tuje kwako bila kuficha chochote ili kurejelea hali ya awali ya mwanadamu ambapo hakuwa na hatia. Tumevaa maringo, kutotii, unyanyasaji na

maovu ambayo yamefanya maisha ya wengine kuwa magumu. Tujengee jamii inayokupendeza na kuwahudumia wengine, kuendeleza umoja na kukuabudu.

KITUO CHA 11: Yesu asulubiwa msalabani

Tunashuhudia akipigiliwa misumari msalabani. Je, tukiutazama uso wake tunaona kama kuna uchungu na dhiki ambayo hawezi kufahamu? Bwana, hata nasi huwasulubisha ndugu zetu, tunakataa kuwasamehe, kuwasaidia au kushirikiana nao kujenga jamii ya upendo. Nyoyo zetu zimejaa chuki na roho wa kisasi. Tusaidie kuachana na yote hayo kwa kusameheana kwani tunaposamehe nasi husamehewa.

KITUO CHA 12: Yesu anakufa msalabani

Tunasimama pale chini ya msalaba na kuukumbatia ukombozi wetu. Hapo, tunashuhudia anayetupatia uhai akiingia katika mauti. Bwana, huwa tunakumbana na vifo vidogo katika chuki, familia zilizovunjika, vurugu na kutoelewana. Ndani ya kila mmoja wetu kuna jeraha la kutofaulu, kuaibishwa na nia mbaya. Kupitia kwa kifo chako, tunaomba utubadilishe ili tuwe chanzo na nguvu za ubunifu ambapo ushirika, urafiki na uelewano zitapata kipa umbele.

KITUO CHA 13: Yesu atolewa msalabani

Tunashuhudia akitolewa msalabani na kutamani kuugusa na kuupapasa mwili wake. Tunakumbuka yote ambayo mikono yake iligusa, wote aliowakumbatia na kuwaletea baraka, tunatafakari na kuacha yote hayo yazame ndani mwetu. Anafahamu muujiza wa mauti. Ameingia katika mikono mizuri. Bwana, tunakumbuka maneno ya mtumishi wako Ayubu. Ninajua kwamba Mkombozi wangu yu hai. Nami baada ya ngozi yangu kuharibiwa, bado nikiwa na mwili huu nitamwona Mungu; mimi nitamwona kwa macho yangu mwenyewe ... (Ayubu 19:25-27). Tusamehe kwa kuwa mara nyingi tunaishi tukijifikiria tu sisi wenyewe; katika maisha yetu, tunajijali tu sisi wenyewe, kazi zetu, tamaa zetu na mambo tunayoyaogopa. Tunaomba upande ndani yetu moyo mkubwa wa kujali na uliojaa ukarimu. Tusaidie kuwajali wote walio karibu nasi.

KITUO CHA 14: Yesu alazwa kaburini

Tunasimama kwa muda nje ya kaburi lake. Safari hii yake ya mwisho duniani imetuonyesha maana ya zawadi yake mwenyewe kwetu. Kaburi lake linawakilisha kila kaburi tinalokabili kwa woga na kung'ang'ana kuamini huenda kaburi halina maiti. Bwana, ulitufundisha kwamba maisha ya milele ni kumjua Mungu na Yesu ambaye alimtuma kwetu. Tupe moyo wa kujitolea, imani na upendo; kujitolea kwa maisha ya wanadamu wote na hasa walio dhaifu na wanyonge. Tusaidie kuonyesha wengine maana ya uhai wa milele, upendo na imani inayotusaidia kushinda woga wa mauti.

Kiongozi: Tunakuhusudu Kristo na kukubariki.

Wote: Kwa sababu kwa msalaba wako umeukomboza ulimwengu.

WIKI YA KWANZA

FAMILIA: MSINGI WA KANISA LETU NA JAMII

TAZAMA: SIMULIZI

Faraja na Fahari pamoja na watoto wao wawili, Amani na Jasiri, waliishi kwa furaha kijijini Chang’omba. Faraja, mfanya biashara aliyefanikiwa, na mumewe, Fahari, aliyekuwa ameachishwa kazi na kampuni moja ya utengenezaji bidhaa, walishirikiana kikamilifu wakati wa furaha na hata wa majonzi. Hata hivyo, dhoruba ilikuwa inajikusanya kuivuruga furaha na amani ya familia hiyo kutokana na shinikizo za jamii na mashaka ya kibinafsi.

Fahari alisumbuka sana kimawazo kutokana na kusutwa na kudunishwa na marafiki zake kwa kumtegemea mkewe kujikimu kimaisha. Hali hii ilimfanya kujiona duni, asiyeweza kujitegemea na kutojiheshimu. Amani na upatanifu katika familia yake ziliathirika.

Binti yao, Amani, alisumbuliwa na kutengana kwa wazazi wake na akajitosa kwa starehe na anasa za marafiki wake wapya waliomvuta kuungana nao kwa ahadi za kumthamini kama mmoja wao. Alinaswa katika mtego wa utumiaji mbaya wa dawa za kulevyu, akaacha shule na kudhoofika kiafya.

Jasiri, katika kukwepa utengano uliokumba familia yake, alijitosa katika masomo na shughuli za ziada shuleni kama vile spoti. Mambo yalizerota zaidi wakati Fahari alimshambulia na kumwumiza Faraja aliyelazimika kulazwa hospitalini.

Hali hiyo ya kuhuzunisha ilimtesa mawazo Jasiri na akaazimia kutafuta wazee wa kanisa waliowapatanisha Fahari na Faraja na kuwakumbusha kuhusu umuhimu wa umoja, heshima na upatanifu katika familia ikiwa ndio msingi wa jamii. Fahari aliahidi kukubali kuendelea kumtegemea mkewe na kuidhinisha kuwa yeye au mkewe angeipatia familia riziki. Waliwaomba radhi watoto wao na wakaahidi kuwa mfano mwema kwao, huku wakijutia madhara waliyowasababishia, hasa Amani waliyemsajili katika kituo cha kumsaidia kuacha utumiaji mbaya wa dawa za kulevyu.

AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Kifungu 45(1) cha Katiba kinaitambua familia kuwa ndicho kitengo cha asilia na kimsingi cha jamii na msingi muhimu katika mpangilio wa jamii. Mara nyingi Baba Mtakatifu Francis amekuwa akisisitiza umuhimu wa familia kama nguzo kuu ya jamii. Amekuwa mtetezi mkuu wa heshima

kwa wote, kusaidiana na kuvumiliana katika kila familia. Ameangazia nafasi ya upendo na uelewano kukabiliana na changamoto za kibinafsi na kijamii. Wito wake kutaka wote katika familia kuheshimiana na kuelewana unaafikiana na uamuzi wa Fahari na Faraja kusameheana kwa upendo na heshima.

Kifungu 27(1) cha Katiba kinasisitiza kuwa kila mtu ni sawa mbele ya sheria na ana haki ya kulindwa na kupata manufaa sawa ya sheria, na hivyo kuakisia umuhimu wa usawa na kuilinda familia. Kulazwa hospitalini kwa Faraja baada ya kushambuliwa na mumewe kunamulika fujo zinazokabili familia. Imani za kitamaduni husisitiza umuhimu wa familia katika kudumisha utangamano wa jamii na upatanisho. Familia za jamii asili za Kiafrika ni chanzo cha nguvu na umoja. Lakini uzingatiaji wake sugu wa hali ya kuwa mwanamume au mwanamke unafichua haja kubwa ya juhudi za kuleta usawa wa jinsia na utangamano kwa familia za Kiafrika.

Mafundisho ya Kanisa Katoliki kuhusu Jamii yanasisitiza umuhimu wa familia kama kitengo cha msingi cha jamii, kuimarisha maadili ya amani, haki na heshima. Familia ni mazingira ya msingi ya malezi ya uadilifu na utakatifu. Mafundisho yanasisitiza pia umuhimu wa heshima kwa binadamu na utakatifu wa maisha. Ndiposa kanisa linalaani dhuluma kwa wanadamu, linaangazia usawa wa wanaume na wanawake kwa heshima, haja ya kujenga mazingira salama na yanayosaidia wote katika familia, na kuhimiza kumalizwa kwa tamaduni finyu zinazoendeleza maovu kama hayo.

TAFAKARI YA KIROHO

Kumbukumbu ya Torati 26:4-10

Waroma 10:8-13

Luka 4:1-13

Tunamwamini Mungu anayetukomboza na kutuongoza nyikani ya maisha yetu ili kuufikia ufanisi anaotamani tuupate. Nguzo kuu ya imani yetu ni ukombozi uliopatikana kwa manufaa yetu. Upendo wake kwetu ni mkuu na yuko tayari kukabiliana na udhaifu wetu na machungu ili kukutana nasi katika hali zetu halisi za maisha, kututia moyo kwa mazito tunayoyapitia, kutuondoa na kutuingiza maishani mapya aliyotuandalia.

Roho Mtakatifu alimwongoza Yesu nyikani ambapo alijaribiwa na ibilisi. Vishawishi hivyo vinadhihirisha hali ya vita vya kiroho ndani yetu na jinsi imani ilivyo na nguvu ya ushindi. Kwa kuishinda njaa, Yesu anatubainishia kuwa riziki yetu hutokana na uhusiano wetu na Mungu wala sio mali za dunia. Familia imara haitegemei tu mahitaji ya mwili na mali ila uhusiano thabiti na Mungu. Ili kukabiliana na hatimaye kushinda

vishawishi vya kufanya miujiza kwa manufaa ya ibilisi na kumjaribu Mungu, Yesu anasisitiza kwamba ulinzi wa Mungu hutokana na imani kwa mapenzi na fadhila zake. Familia hulindwa ikidumisha imani yake kwa Mungu. Yesu anasisitiza ni Mungu pekee anayefaa kusujudiwa. Hatufai kamwe kuchagua ufalme wa muda wa dunia badala ya ufalme wa milele wa Mungu.

Ibilisi huzitia familia katika vishawishi na kuiacha njia ya Mungu. Hata hivyo, kama alivyotonyesha Yesu, imani yetu imara kwa Mungu itatuwezesha kushinda majaribu. Familia haina budi kutegemea maandiko matakatifu kuongozwa na kupata nguvu za kukabiliana na majaribu. Tukiyaafahamu majaribu ya Yesu, tutavielewa kikamilifu vishawishi vyetu katika dhambi na kujifunza jinsi ya kukabiliana navyo kwa imani na kumtegemea Mungu.

Kwa hivyo, Yesu anataka kukutana nawe na kukukomboa kutoka nyikani yoyote ambayo familia yako inapitia.

TENDA: MASWALI YA KUWAZIA

- » Je, maisha na miundo ya familia huathiriwa kwa njia gani na masuala ya kiuchumi, kijamii, kitamaduni na kisheria?
- » Je, tunaimarisha amani na upatanifu katika familia?
- » Familia, kanisa na jamii zinatekeleza wajibu gani katika ukuaji wa watoto?

KUJICHUNGUZA

- » Je, ninahimiza upatanifu na uelewano katika familia yangu?
- » Je, mimi ni mzushi au mtatuzi wa shida katika familia yangu?
- » Je, mimi ni mfano wa kuigwa katika familia yangu na kwenye jamii?
- » Je, ninahimiza maadili bora ya familia katika jamii?

MATENDO YALIYOPENDEKEZWA


- » Fanya majadiliano ya kila mara na ya wazi na familia.
- » Shauriana na wataalamu wa ushauri wa masuala ya maisha ya familia kuhusu kuwaandaa wanaopanga kufunga ndoa na ushauri wa kuimarisha maisha ya wanandoa.
- » Imarisha vikao vya sala za kila siku kwenye familia na mshirikiane kwa chakula na kazi.
- » Andaa mipango ya maisha ya familia.



Eneo bunge la Parachichi


Bw. Tikititi

MIEZI MICHACHE BAADAYE



JELA LENYE ULINZI MKALI

Ufisadi ni sarafini katika kiini cha Jamii ambayo huangamiza maadili ya jamii



MIAKA MICHACHE BAADAYE

Eneo bunge la Parachichi

Makazi ya Tikititi

Eneo bunge la Parachichi

HATIMAYE

MAJI

JISI KUU

HOSPITALI

JISI KUU

MP

JISI KUU

TAZAMA: SIMULIZI

Tikiti alikuwa mzee wa kijiji aliyeheshimika kote katika eneo bunge la Parachichi kwa kuisaidia jamii yake katika miradi ya maendeleo. Alishikilia nyadhifa za uongozi kwenye jamii na kanisa. Uchaguzi mkuu ulipofanyika, aligombea ubunge, akaahidi mengi ya kuinua maisha na hali za wapigaji kura na akachaguliwa kwa kauli moja kwa sababu wote walimwamini.

Miezi michache baada ya kuchaguliwa, Tikiti alianza kuwaonyesha raia ujeuri, kiburi, hasira na kukosa uvumilivu. Alikoma kushiriki katika shughuli za jamii na kufuja rasilmali zilizopaswa kuifaidi jamii. Alijipatia msafara wa magari na kuhamishia familia yake jijini. Alitumia ushawishi wake kuhakikisha mwanawe mkubwa, Wadonjo, ameteuliwa kuiongoza kamati ya hazina ya maendeleo ya Parachichi ya ununuzi wa bidhaa na huduma. Kijana aliitumia fursa aliyopewa na babake kufuja pesa za karo za watoto maskini na ujenzi wa barabara, shule na hospitali. Alinunua ardhi mtaani mmoja wa kifahari jijini na kujenga nyumba za kukodisha.

Tikiti alikuwa mwenyekiti wa kamati ya bunge ya bajeti iliyopendekeza kodi za juu za kuumiza raia kwa kuongeza gharama ya maisha. Kamati ilipendekeza ada mpya kuwawezesha wabunge kuishi kwa raha, anasa na kutumia vibaya mali ya umma. Kamati ilialika maoni ya raia kuhusu kodi zilizopendekezwa lakini yalipuuzwa na bajeti ikapitishwa bila kufanyiwa badiliko lolote.

Watu wa Parachichi waliomba idara ya kupigana na ufisadi kuchunguza utumiaji mbaya wa pesa za eneo bunge lao na hatimaye wakachukua hatua za kumng'oa Tikiti mamlakani. Tikiti na mwanawe walishtakiwa mahakamani, wakapatikana na hatia ya makosa ya kiuchumi na kuhukumiwa kufungwa jela. Serikali ilitwaa mali zao na kufunga akaunti za banki.

AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Ufisadi ni utumiaji mbaya wa mamlaka kwa manufaa ya kibinafsi. Unaweza kuwa wa kiwango kidogo, kikubwa au ulioenea katika ngazi zote za mamlaka kulingana na kiasi cha pesa na mali zinazopotea. Ufisadi huathiri jamii na kudhoofisha imani ya raia kwa mifumo ya kisiasa na kiuchumi, mashirika, na viongozi na huwanyima watu uhuru,

huduma muhimu kama za afya, pesa na hata kusababisha vifo. Ovu hilo hudunisha pia kiwango cha bidhaa na huduma kwa umma kwani rasilimali hutumiwa kwa mahitaji ya binafsi badala ya kuwekezwa kwa maslahi ya umma. Gharama ya bidhaa na huduma huongezeka, raia hupoteza muda mwingi wakizitafuta na wasio na uwezo wa kutoa hongo husumbuka wakitafuta kuhudumiwa. Isitoshe, ufisadi hudhoofisha haki na kuwanyima wengi nafasi sawa, unaendeleza migawanyiko ya kijamii na kuimarisha uhasama wa kidini na kikabila. Kadhalika, hudunisha demokrasia kwa kuwafanya raia kutokuwa na imani na asasi za umma, na kudunisha uongozi wa sheria. Hukwamisha maendeleo ya kiuchumi kwani badala ya rasilimali kutumika kuwekeza katika shughuli za uzalishaji mali, hutumiwa kuendeleza ubepari kwa misingi ya mapendeleo ya kindugu na marafiki, kuzidisha hali ya kutokuwa sawa na kueneza mizizi ya umaskini.

Shirika la Transparency International katika ripoti yake ya 2023 kuhusu utambuzi wa ufisadi, lasema Kenya ni miongoni mwa mataifa 54 yenye viwango vikubwa vya ufisadi duniani. Sura ya Sita ya Katiba inaangazia uongozi na maadili. Inaweka taratibu za kubuni asasi muhimu za kukabiliana na ufisadi nchini. Kenya ina historia ndefu ya kashfa za ufisadi ambazo hunufaisha watu binafsi. Mashirika ya kupambana na ufisadi hayajafanikiwa pakubwa katika kukomesha ovu hilo.

Hakuna rais ambaye uongozi wake umeepuka kashfa ya mahindi tangu 1963. Mnamo 1965, Kenya iliuzia Japan magunia 250,000 ya mahindi. Muda mfupi baadaye, Serikali ililazimika kuagiza maelfu ya tani za mahindi ya manjano kutoka Marekani. Kati ya 2008 na 2009, Kenya ilikabiliwa na kashfa ya mahindi ya kutoka nje. Kashfa ya majuzi ya fatalaiza inatukumbusha kuhusu ile ya KenRen ya miaka ya 1970 ambapo Wakenya walipoteza Kshs2.4 bilioni. Miaka ya 1980 na 1990 ilishuhudia kashfa ya Goldenberg iliopokonya umma dola bilioni 1.5. Gharama ya mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia maji wa Turkwell ulioanzishwa 1986 iliongezeka maradufu hadi dola 450 milioni. Kashfa ya Anglo-Leasing ya mapema miaka ya 2000 iligharimu Wakenya karibu dola milioni 33. Kashfa ya mafuta ya Triton ilizamisha dola milioni 100. Mamilioni ya pesa za mpango wa elimu ya msingi bila malipo (FPE) ulioanzishwa 2003 yalifujwa. Mnamo 2014, Kenya ilikopa dola bilioni 2.75 kwa hati dhamana ya kimataifa ya Eurobond. Lakini inadaiwa haijulikani jinsi kiasi kikubwa cha pesa hizo kilitumika. Kshs791 milioni za National Youth Service (NYS) zilipotea 2015 kupitia kwa kandarasi bandia. NYS ilipoteza kitita kingine cha Kshs9 bilioni kwa miradi hewa. Katika msimu huo huo, Wizara ya Afya ilipoteza shilingi bilioni tano za hospitali, dawa na muundo msingi. Mradi mkubwa wa Galana-Kulalu uliokusudiwa kutosheleza Wakenya kwa chakula

kwa kunyunyuza maji mashamba ya ekari milioni moja, ulimeza shilingi bilioni 7.3. Katika kashfa ya mradi wa mabwawa ya Arror na Kimwarer ambayo hayakujengwa, kampuni husika ililipwa Kshs 63 bilioni. Kashfa ya karibuni ni ya Adani ya kuupanua uwanja wa ndege wa Jomo Kenyatta (JKIA) ambayo imefutuliwa mbali. Umma ulipoteza Kshs10 bilioni mnamo 2010 katika kandarasi sawa ya JKIA.

Baba Mtakatifu Francis alipozuru Kenya 2015, aliwahimiza Wakenya kuepukana na ufisadi. Akiwahutubia vijana, alisisitiza: “Ufisadi si njia ya uhai ila ni njia ya mauti. Kila mara tunapochukua hongo na kuiweka mfukoni, tunaharibu nyoyo zetu, nafsi zetu na nchi yetu. Tafadhali tusijenge ladha ya hiyo sukari iitwayo ufisadi na rushwa.”

Katika waraka wake kitume, *Evangelii Gaudium*, Baba Mtakatifu Francis amesisitiza madhara ya ufisadi kwa jamii, akisema: “Ufisadi ni kansa iliyoingia katika kiini cha jamii na kuangamiza msingi wa maadili wa taifa.” Anawahimiza waumini wote kuepuka ufisadi na kujitahidi kujenga jamii inayojali haki. Baadaye Oktoba 5, 2019, Baraza la Maaskofu Wakatoliki Kenya lilizindua kampeni ya kupigana na ufisadi, *Na tuuvunje mnyororo wa ufisadi*, na kuwaongoza maelfu ya waumini kuweka ahadi ya binafsi ya kupigana na ufisadi.

Kushiriki kwa umma ni mojawapo ya misingi ya Katiba na kanuni za uongozi inayohitaji kushika mizizi. Pesa zinafaa kukusanywa na kutumika kulingana na mahitaji ya jamii. Isitoshe, umma unafaa kusimamia matumizi ya pesa hizo na kuhakikisha ubora wa miradi.

Pana haja ya kukabiliana na ufisadi na kutekeleza kikamilifu sheria za kupambana na ovu hilo. Wakenya hawana budi kuzungumza kwa sauti moja na kuhimiza uwajibikaji kwa rasilimali za nchi. Hilo linaweza tu kutimia umma ukishiriki kikamilifu katika usimamizi wa rasilimali na kuheshimiwa kwa uongozi wa sheria.

TAFAKARI YA KIROHO

Mwanzo 15:5-12, 17-18

Wafilipi 3:17—4:1 or 3:20—4:1

Luka 9:28b-36

Abrahamu aliziamini ahadi za Mungu za mambo ambayo kwa wanadamu zilionekana kama hazingetimia. Uadilifu wake, uaminika na unyenyekevu zilimpelekea kupendwa na Mungu. Mtu aliye na sifa kama hizo hawezi kuwa mfiadini kwa sababu anawajibika kwa Mungu. Huwa tunanaswa na mtego wa ufisadi tunapokosa kumkabidhi Mungu mahitaji yetu. Ili kuuepuka mtego huo, tuache kuthamini mambo ya dunia hii

kama anavyoshauri Paulo katika somo la pili, na kutokubali kuwa watumwa wa mambo hayo. Tuangazie thamani yetu kamili ambayo ipo mbinguni ambapo tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo.

Katika Injili, Yesu anawapeleka Petro, Yohana na Yakobo mlimani ili kuushuhudia utukufu wake. Safari ya kuufikia utukufu wa Mungu ni ngumu na yahitaji uvumilivu. Tunapouanza msimu wa Kwaresima, tunatafakari kuhusu utukufu wa Mungu unaotutia nguvu za kuvumilia mazito ya misalaba tunayobeba. Ni muhimu kuishi tukizingatia uadilifu, bila kujali changamoto zake kwani haziwezi kulinganishwa na neema tutakazopata duniani na utukufu tulioahidiwa mbinguni.

Tujitahidi kuushuhudia utukufu wa Mungu kama walivyofanya Petro, Yohana na Yakobo na tusisahau kuwa hiyo ndiyo ahadi ya wanaovumilia hadi mwisho.

TENDA: MASWALI YA KUWAZIA

- » Umekumbana na ufisadi wa aina gani katika familia, kazini, jumua na kitaifa?
- » Unafahamu kuwa ufisadi ni dhambi kubwa mbele ya Mungu wa haki na ubinadamu?
- » Ufisadi na ulafi zinaathiri vipi familia, jamii na nchi?
- » Wewe binafsi unatekeleza wajibu gani kuimarisha vita ya kupambana na ufisadi? Unafahamu kwamba ufisadi ni ovu?

KUJICHUNGUZA


- » Je, nimehusika na matendo ya ufisadi?
- » Je, nimefaidika kutokana na shughuli yoyote ya kifisadi?
- » Je, nimechukua hatua gani kuikata minyororo ya ufisadi?

MATENDO YALIYOPENDEKEZWA

- » Tubu, uachane kabisa na ufisadi na uwe mwaminifu kwa familia yako.
- » Shiriki kikamilifu katika harakati za kupigana na ufisadi.
- » Andaa warsha za kuelimisha watu kuhusu ufisadi na madhara yake.
- » Hudhuria na ushiriki katika shughuli za umma za kuandaa na kusimamia bajeti.

WATU MILLION **47** KENYA

Wakenya wasio na ajira



25% wengine

VIJANA WA KATI YA MIAKA 18 na 35

75%

Imani kali za dini



Uhalifu



Vijana 50,000 wanaoifimu vyyo vikuu kila mwaka




HIV & AIDS




Utumiaji mbaya wa dawa za kulevya na pombe



Biashara hatamu



Uchumi mbaya



Kifuo Cha kuwaimua vijana



Kifuo Cha kuwaimua vijana



Usirikika wa umma



wavumbuzi



Wenye ujuzi wa teknolojia

Wenye aya na nguvu

VIJANA.KE

Wenye talanta

wajioelimika

wajiowezeshwa

WIKI YA TATU

VIJANA: RASILIMALI ISIYOTUMIKA IFAAVYO

TAZAMA: SIMULIZI

Tangu kuzaliwa, Shupavu alikuwa kijana mchangamfu aliyependwa na wazazi wake waliokuwa wakazi wa kijiji cha Tayari. Akitoka shule, alizoea kuchunga mifugo wa wazazi wake na kuogelea mtoni. Alipenda kuhudhuria Misa kanisani ya kijiji chao na wengi walimwita 'Askofu' kwani kwa muda mrefu alikuwa mtumishi wa misa. Alipohitimu shule ya upili, Shupavu alifuzu kujiunga na chuo kikuu kwa kozi ya sayansi ya kompiuta. Akiwa mwingi wa matumaini na ndoto, alisafiri kuelekea jijini kwa mara ya kwanza, akiahidi familia kuirudia akiwa mtu bora zaidi.

Alimaliza masomo yake akiwa nambari moja darasani na alikuwa tayari kuchangia kuubadilisha ulimwengu akitumia maarifa na ujuzi aliojipatia. Lakini mwaka mmoja baada ya kupata digrii, Shupavu hakuwa bado ameajiriwa kazi. Biashara ndogo aliyoianzisha mtandaoni iliporomoka serikali ilipoanza kutoza ushuru biashara zote za mtandaoni. Nyumbani, wazazi na ndugu zake walisubiri awasaidie. Nduguye mdogo alikaribia kujiunga na shule ya upili na dadake alifukuzwa shule kwa kukosa karo. Shupavu alikuwa tegemeo lao kwani babake mkongwe hakuwa na nguvu tosha za kuikimu familia.

Shupavu alizidi kukata tamaa kiasi cha kukosa wasaa wa kwenda Misa kwani alitumia muda wake mwingi kujitafutia riziki yake pamoja na ya familia. Siku moja akitembea barabarabi za jiji, alikutana na Ovu aliyekuwa mwanafunzi mwenzake katika chuo kikuu. Ovu alikuwa akiendesha gari kubwa la kifahari na aliandamana na msichana mrembo. Bila shaka, maisha ya Ovu yalikuwa mazuri, ingawa hakufuzu chuo kikuu; aliacha masomo kwa kucheza kamari. Shupavu hakuamini jinsi maisha yake yalimkalia ngumu ilhali alipata matokeo mazuri shuleni na chuoni. Ovu alimwalika Shupavu afisini mwake na akamweleza kuhusu biashara ya kuuza na kununua pesa za kigeni mtandaoni. Shupavu hakujua ameingizwa katika shughuli haramu ya ulaghai na wizi wa pesa. Baada ya muda mfupi, Shupavu alianza kupata pesa zilizomwezesha kuishi kwa anasa, kufanya sherehe, kulewa pombe na kuvuta sigara. Mambo yalimwendea mrama polisi walipovamia afisi zao na kuwanasa Shupavu na wenzake kwa kufanya biashara haramu mtandaoni.

Safari ya kwanza jijini ya wazazi wa Shupavu ilikuwa ya kumkaribisha kutoka jela alipomaliza kutumikia kifungo cha miaka minne. Alikuwa

amedhoofika, hakuzungumza sana wala kuingiliana na wengine kwa urahisi. Nyumbani, alirejelea utumishi wa kanisa ambapo kupitia kwa mradi wa kuwainua vijana, alipata mafunzo ya kilimo na masoko. Alitumia maarifa hayo kuanzisha tovuti ya kuwawezesha wafugaji kijijini kupata kwa urahisi masoko ya jijini. Shupavu akawa mlezi na mwalimu wa vijana katika jamii.

AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Kifungu 260 cha Katiba kinaeleza kuwa vijana ni ujumla wa watu wote katika Jamhuri ambao wametimiza umri wa miaka 18 lakini hawajatimiza umri wa miaka 35. Wakenya milioni 37, au asilimia 70 ya watu milioni 47 waliokadiriwa kuwa nchini kwa mujibu wa sensa ya 2019, walikuwa na umri wa chini ya miaka 35. Idadi ya kundi hili inatarajiwa kuongezeka zaidi siku za usoni na huenda ikafika asilimia 80, na hivyo basi kuipatia Kenya nafasi maalumu za kijamii na kiuchumi, na wakati huo huo kutoa changamoto kama vile uhaba wa nafasi za kazi.

Katika siasa, vijana walikuwa asilimia 39.7 ya wapigaji kura waliojiandikisha 2022. Idadi ya vijana waliochaguliwa kushika nyadhifa tofauti imeongezeka kutoka 317 mnamo 2017 hadi 335 kufuatia uchaguzi mkuu wa 2022.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa Julai 2023 na Tume ya Elimu ya Vyuo Vikuu (CHE), jumla ya vijana 50,000 huhitimu kutoka vyuo vikuu kila mwaka. Wengine maelfu hupata mafunzo vyuoni vingine, ikiwa ni pamoja na vya mafunzo anuai ya kiufundi. Vijana wote hao wana ustadi wa kiufundi, maarifa na ujuzi wa kiwango cha juu. Lakini wote wanakabiliwa na ukosefu wa ajira na kusababisha kuongezeka pakubwa kwa idadi ya vijana wasio na kazi. Asilimia 67 ya watu wasio na kazi ni vijana. Na hata wakiajiriwa, vijana wengi hubaguliwa kazini, hali inayowaletea matatizo ya akili na kuwakatisha tamaa maishani.

Maishani, vijana wamejipata katika njia panda ya matarajio makubwa ya jamii, na uhaba wa nafasi za ajira. Tatizo hili limesukuma wengi wao kutumia vibaya dawa za kulevya na pombe, kuingilia uhalifu (mitandaoni au kujiunga na magenge), na uzinzi unaowaletea magonjwa ya zinaa. Wengine wameambukizwa na kuambukizana virusi vya HIV na Ukimwi. Kuna walioingilia madhehebu yenye imani kali, wengine wanatumiwa vibaya na wanasiasa, huku wengine wakianzisha familia zisizo thabiti. Changamoto hizi zimewatatiza vijana na kuwanyima nafasi wanayostahili ya kuutumia kikamilifu uwezo walio nao kuendeleza uzinduzi wakitegemea afya na nguvu za ujana, upana wa maarifa, talanta na elimu yao ya juu. Sera ya Ustawi

wa Vijana Kenya ya 2019 inatambua kanuni za Katiba katika Kifungu 55 zinazoitaka Serikali kuchukua hatua, ikiwemo miradi ya vitendo sawazishi, kuhakikisha vijana wanapata elimu na mafunzo yanayofaa; wana fursa ya kujumuika, kuwakilishwa na kushiriki nyanjani za kisiasa, kijamii, kiuchumi na nyanja nyingine za maisha; wanapata kazi; na kulindwa dhidi ya tamaduni zinazodhuru na kunyanyasa.

Pana haja kubwa ya kuwafahamisha vijana zaidi kuhusu uwezo walio nao wa kuijenga jamii kwa kushiriki katika taratibu za kidemokrasia. Ingawa vijana ndio wengi Kenya, idadi ndogo ya waliojiandikisha kuwa wapigaji kura ni thibitisho la jinsi wamepuuza nafasi waliyo nayo ya kuchagua viongozi vijana kuwatetea. Vijana wana uwezo mkubwa lakini wakikosa mwelekeo kamili wa kimaadili na kiroho, wanaweza kusababisha madhara makubwa.

Suala muhimu la mambo ya roho miongoni mwa vijana halifai kupuuzwa. Baba Mtakatifu akifunga Misa ya Siku ya Vijana Duniani ya 2019 katika Panama City alisema: "Vijana wapendwa, ninyi sio tegemeo la baadaye lakini tegemeo la sasa la Mungu."

TAFAKARI YA KIROHO

Kutoka 3:1-8a, 13-15

1 Wakorintho 10:1-6, 10-12

Luka 13:1-9

Maisha ya Musa yanatufundisha jinsi Mungu anavyomsubiri mtu nyikani tofauti za maisha na kumwandaa kuwa mtumishi wake. Huwaonyesha wote uwezo mkubwa walio nao na anavyotaka wautumie. Vijana wana uwezo ambao mara nyingi tunaupuza. Katika nyika ya maisha yetu, mambo yakituendea mrama, Mungu aliyetuumba na atatukiaye mema hutuinua. Tukinyenyekea kwake, atatukomboza na kutuonyesha rasilimali za uadilifu alizotupatia ambazo hatujazitumia kikamilifu, na hatimaye kututuma kuwa wafanya kazi shambani lake la mizabibu. Tunahitaji unyenyekevu kama huo ili kuuona uwezo wa vijana ambao haujatumika kikamilifu.

Maisha yetu na pia yale ya vijana wetu yanahitaji huruma za Mungu na kuzalisha maadili. Isitoshe, ni lazima tuwe tayari kupunguziwa yote yasiyotakikana maishani kama vile hisia za chuki zisizo na sababu ambazo hutuzuia kutambu a uwezo walio nao vijana. Ingawa Yesu ndiye mkulima maishani yetu, hata sisi tu wakulima kwani ni lazima tushirikiane na Bwana, tukitegemea nguvu za aliyetuumba ili kuhakikisha ukuaji imara wa mambo yetu ya kiroho na hivyo kuhakikisha matunda ya uadilifu yanazaliwa maishani mwetu.

Hata baada ya dhambi kututenganisha na Mungu, hakutuangamiza. Alimtuma Bwana wetu mwenye huruma na upendo kutuokoa na kutupatia nafasi moja zaidi. Mungu wetu hufanya kila juhudi kutuokoa.

Tushirikiane naye kwa sala za kila siku, tutii amri zake, tufanye matendo ya upendo wa hiari na tujitoa kwake. Hatimaye, tukimruhusu Bwana kufanya yote anayokusudia kwetu, maisha yetu yatazaa matunda mema.

TENDA: MASWALI YA KUWAZIA


- » Unayaelewa majukumu na nafasi za vijana Kenya?
- » Ni vitisho gani ibuka vinavyowazuia vijana kuutambua uwezo wao kamili?
- » Mashirika ya serikali na yasiyo ya serikali yamewapa vijana nafasi gani kuwawezesha kugundua uwezo wao kamili?
- » Ni hatua gani zinahitajika kuimarisha ushirika wa vijana katika taratibu za kidemokrasia?
- » Kanisa limeshughulikia kikamilifu masuala ya vijana?
- » Familia huwasaidiaje vijana katika mambo ya kiroho?

KUJICHUNGUZA

- » Je, nimeyashughulikiaje masuala yanayokabili vijana katika jamii?
- » Je, huwa ninawahusisha vijana katika taratibu za kuchukua maamuzi katika ngazi zote?
- » Je, huwa ninashiriki shughuli za demokrasia za ngazi zote?

MATENDO YALIYOPENDEKEZWA

- » Andaa vikao vya kuelimisha vijana kuhusu demokrasia katika ngazi za familia, parokia, jamii na kitaifa.
- » Anzisha hazinadata ya vijana, kituo cha kuwafaa na mradi wa jamii wanaousimamia kuwawezesha kujipatia mapato.
- » Yashughulikie mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiroho na kiakili ya vijana.
- » Kanisa liangazie masuala ya vijana na kuwahubiria.



Baada ya ukuru

1-4-2-3

8-4-4

2-6-3-3-3 (CBC)

SHULE.ke

Afisi ya wapokezi

Karo ya Shule

Haki ya elimu

Kukuza vipawa

ELIMU.ke

Vyuo vya serikali na mashirika ya dini

Elimu isiyo na malipo kwa wote

Sera kamili

Teknolojia ya kisasa

Hazina ya kufosha na inayogawitwa wote kwa usawa

MUUNDO msingi unaofaa

Idadi ndogo ya wanaopata elimu ya juu

Umaliwu

Kuzoresha kwa maadili

Ukosefu wa ajira

WIKI YA NNE

WAJIBU WA ELIMU YA MKABALA WA JUMLA

TAZAMA: SIMULIZI

Rima alilelewa katika jamii ya Elimu iliyosifika kwa matokeo yake bora masomoni, taratibu thabiti na vyuo vyenye usimamizi wa hali ya juu ipasavyo. Alikuwa msichana mchangamfu aliyependa kucheza tenisi, kusoma, kuandika hadithi fupi, kuimba na kucheza dansi. Alikuwa pia katika kundi la vijana Wakristo akiwa mmoja wa maafisa wake wakuu.

Rima alisoma kwa bidii na kushikilia nafasi ya kwanza darasani. Alipata alama za juu katika mtihani wake wa mwisho wa shule ya msingi na kufanikiwa kujiunga na mojawapo ya shule kubwa za sekondari za umma. Rima alikuwa bingwa masomoni, michezoni na mambo mengine ya kufanikisha jamii kutokana na malezi bora ya wazazi wake, na utunzaji wa walimu, viongozi wa dini na jamii.

Rima alitamani sana kuwa rubani wa ndege. Kipawa chake cha tenisi kilizidi kukua na akaiwakilisha jamii yake katika mshindano tofauti ya kitaifa na kimataifa. Akijiandaa kwa mtihani wa mwisho wa sekondari, Serikali ilizindua mabadiliko katika elimu ambayo yalifungia watoto wengi maskini nafasi za elimu ya juu. Baada ya mtihani, Rima alijiunga na mojawapo ya vyuo bora nchini vya mafunzo ya urubani lakini akashindwa kupata mkopo wa serikali kumwezesha kulipa karo na kuendelea na masomo. Kwa bahati nzuri, alipata nafasi ya kwenda kusomea ng'ambo bila malipo kutokana na ustadi wake wa tenisi.

Wanafunzi wengine wa jamii ya Elimu hawakuwa na bahati kama Rima, na hazina ya serikali ya masomo ya juu haikuwasaidia. Viongozi wa dini walilalamika kuhusu kuzorota kwa kiwango cha elimu na kuitisha kikao cha mashauriano na wadau wote. Waliohudhuria walikubaliana kwamba kila mmoja atekeleze wajibu wake kikamilifu. Wadau wote waliunga mkono kauli hiyo na matokeo yake yakawa kurejeshwa kwa kiwango cha elimu kitaifa. Matokeo ya mitihani yaliimarika na idadi ya wanafunzi waliojiandikisha shuleni ikaongezeka. Jamii kwa jumla ikaendelea kupata viongozi wasifika na waliowajibika.

AMUA: UTATHMINI WA HALI HALISI

Kifungu 53.1b cha Katiba kinatambua elimu kuwa haki ya msingi ya kila mtoto. Sheria ya Elimu ya 2013 inalinda haki za kila mtu kupata elimu bila kujali hali au tabaka.

Kabla ya uhuru, elimu ilikuwa kipaji cha wenye uwezo na wakoloni kwa manufaa ya serikali ya kikoloni. Baada ya uhuru, serikali ilifanya kila juhudi kuhakikisha kwamba elimu inawashirikisha wote. Ilizindua harakati za kuimarisha elimu kupitia kwa juhudi za harambee zilizoweza maeneo mengi kuanzisha shule za jamii. Jitihada hizo zilisababisha ongezeko la idadi ya Wakenya waliopata nafasi za kusoma na kuhakikishia wote katika jamii nafasi sawa za kusoma.

Kenya imepiga hatua kubwa tangu uhuru kuhakikisha nchi ina mfumo wa elimu unaonufaisha raia wote. Hata hivyo, mifumo yote ya elimu iliyotaribiwa imekuwa na changamoto kwani haijatosheleza kikamilifu mahitaji ya nchi. Imetoa watu wasio na maarifa na ujuzi unaolingana na mahitaji yanayozidi kubadilika ya tasnia mbali mbali, na hivyo basi kusababisha tatizo la idadi kubwa ya watu wasio na ajira.

Tangu ilipopata uhuru, Kenya imetekeleza mfumo wa elimu wa 7-4-2-3 (miaka saba ya elimu ya msingi, minne ya sekondari, miwili ya shule ya upili na mitatu ya chuo kikuu) kuanzia 1963 hadi 1984; mfumo wa 8-4-4 (miaka minane ya elimu ya msingi, minne ya sekondari na minne ya chuo kikuu) kuanzia Januari 1985 kwa lengo la kuwapatia wanafunzi ujuzi na maarifa ya kuwawezesha kujijiri; na tangu 2017 nchi imeng'ang'ana na mfumo wa CBC wa 2-6-3-3-3 (miaka miwili ya elimu ya chekechea, sita ya msingi, mitatu ya sekondari, mitatu ya shule ya upili na mitatu ya chuo kikuu). Hata hivyo, CBC na mfumo mpya wa kugharamia elimu ya vyuo vikuu zimesababisha mashaka na utata miongoni mwa wazazi, walimu, wanafunzi na wadau kwani miundo ya utekelezaji inayozingatwa na serikali haeleweki wazi. Ufumbuzi unaweza kupatikana kwa kushirikisha wahusika wote wakuu na wadau.

Taasisi za mashirika ya dini zimeteteleza wajibu muhimu katika kutoa elimu kwa Wakenya tangu kabla ya uhuru. Lakini mnamo siku za karibuni, wajibu wa dini katika elimu na uandalizi wa sera umeendelea kuwekwa pembeni. Matokeo yake yamekuwa ni kuzorota kwa kiwango cha maadili katika taasisi za elimu. Ingawa maendeleo ya teknolojia yanazinduliwa kila kukicha, huku akili mnemba (AI) ikichukua mahala pa mifumo ya elimu katika sehemu nyingi za ulimwengu, Kenya bado haijakumbatia pakubwa maendeleo hayo.

Kanisa limeendeleza juhudi za wazi za kuimarisha elimu kote ulimwenguni. Baba Mtakatifu Francis katika ujumbe alioutoa Februari, 2024, kwa washiriki wa mkutano wa kuangazia kujitolea kwa Kanisa katika elimu uliofanyika Madrid, Uhispania, alieleza umuhimu wa asasi za Kanisa Katoliki katika kuhakikishia wote nafasi za kusoma. Alikumbusha walimu Wakatoliki katika Uhispania kwamba kanisa

limeitwa kuimarisha elimu shirikishi ambayo inawezesha wanafunzi wote kuonyesha uwezo wao bila kujali hali zao kijamii na kiuchumi, jambo ambalo ni kiungo muhimu cha wito wa elimu wa kanisa wa kuleta matumaini katika juhudi za walimu na wanafunzi kuchangia kuijenga upya jamii. "Ninawakumbuka watoto na vijana wengi ambao hawana nafasi za elimu katika sehemu tofauti za ulimwengu, wanaoathiriwa na unyanyasaji, na hata vita na vurugu."

TAFAKARI YA KIROHO

Yoshua 5:9a, 10-12

2 Wakorintho 5:17-21

Luka 15:1-3, 11-32

Wana wa Israeli walipofika Kanaani na kupiga hema baada ya kusafiri jangwani kwa miaka 40, kuna kanuni ambazo lazima wangezitimiza. Walianzisha maisha mapya ya imani wakiongozwa na kanuni kutoka kwa Mungu. Mfumo wa kweli wa elimu hutuongoza kutoka kwa maisha yasiyo na kanuni na kutuingiza maishani yanayoongozwa na maadili ya Mungu. Tunakuwa viumbe wapya walioyaacha ya kale (2 Wakorintho 5:17) yaliyoongozwa na tamaa ya mali, na kukumbatia maadili mapya ya imani, matumaini na upendo tunayopewa na Mungu.

Mara nyingi, mambo tunayoyachagua hutuingiza dhambini. Kiburi hutufanya tusikiri dhambi zetu na kuishia kuzitetea. Sisi ni wenye dhambi wanaomkaribia Yesu kwa sababu ya njaa ya kiroho, sawa tu na ya mwana mpotevu. Tuna mengi tuliyoyafanya lakini tunajuta. Hatujaridhika maishani na tunatafuta njia ya kujikomboa, sawa tu na alivyokuwa mwana mpotevu aliyemwacha babake aliyempenda. Usimulizi wa Yesu kuhusu mwana mpotevu unafaa kutujaza matumaini kwamba hata nasi tunaweza kushiriki katika sherehe ya furaha, sawa na aliyoandaliwa mwana mpotevu kwa ukarimu.

